TUME YA KIKRISTO YA HUDUMA ZA JAMII

MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA MAKANISA KANDA YA KASKAZINI

MTIHANI WA UTAMIRIFU KIDATO CHA SITA 2023

121/2 KISWAHILI 2

MWONGOZO WA USAHIHISHAJI

1.Mtahiniwa alitakiwa kutoa tofauti tatu kati ya majigambo na mashairi na mfanano uliopo kati ya majigambo na mashairi kwa hoja mbili

MFANANO

- Vyote ni vipera vya ushairi
- Zote hutumia lugha ya picha na tamathali za semi
- Zote zinalenga kuelemisha na kuburudisha jamii (nyongeza)

UTOFAUTI

- Katika majigambo mjigambi hutumia nafsi ya kwanza wakati mashairi hutumia nafsi zote tatu
- Majigambo hayabanwi na kanuni ya urari wa vina na mizani wakati katika mashairi hasa ya kimapokeo yanabanwa na kanuni ya urari wa vina na mizani
- Majigambo hutolewa na mtu kwa lengo la kujigamba au kujitapa kwa lengo la kujisifu wakati mashairi hakuna kujitapa.
- Majigambo ni maigizo ya kujisifu huwasilishwa kwa njia ya maigizo wakati mashairi hayawasilishwi kwa njia ya maigizo(nyongeza)

(hoja 5@2

2. Mtahiniwa anapaswa kutoa maana ya dhana zifuatazo kwa kutumia mifano

i. Tamthilia ni utungo kwa kidrama ulioandikwa ili utendwe jukwaani au usomwe kwa lengo la kutoa maudhui au ujumbe. Mfano tamthilia ya ngoswe n.k

ii. Mizungu ni kauli yenye picha za mafumbo na inayoonyesha ukinzani wa fikra au matukio. Mfano embe limeiva nyumbani ila nashindwa kulila

iii. Misemo ni fungu la maneno linalotumiwa na jamii ya watu kwa namna maalumuili kutoa maana Fulani. Mfano mtu kwao, elimu ni bahari

iv. Hekaya ni kisa kifupi kilichokusudiwa kubaini hekima au funzo Fulani. Mfano Isa (Yesu)

v. Utani ni hali ya kufanyiana mizaha au masihara baina ya watu ambapo hali hii ni tofauti na desturi za kutoheshimiana. Mfano baina ya kabila na kabila au ukoo na ukoo

Hoja 05@ 02

3. Mtahiniwa aeleze mihula minne ya maendeleo ya ushairi wa Kiswahili

a) Muhula wa urasimi karne ya 14-19

Ni muhula uliotawaliwa na tungo nyingi za tenzi mfano;tambuka,hamzia,mwanakupona na shufaka.Katika muhula huu kanuni za utunzi wa mashairi ziliwekwa na ndio muhula ushairi ulitamalaki na kuandikwa sana.

- Muhula wa utasa 1885-1945

Ni muhula ambao ulitawaliwa na maandishi machache ni kipindi cha mabadiliko ya kiutawala na elimu.Ambapo kulikuwa na kubadilika kwa hati ya maandishi kutoka hati ya kiarabu kwenda ya kirumi.Katika kipindi hiki kanuni za uandishi wa maishairi ulianza kupotea.

- Muhula wa urasimi mpya 1945-1960

Ni kipindi cha kufafanua kanuni za utunzi wa ushairi.Katika kipindi hiki kitabu cha sheria za kutunga mashairi kiliandikwa wakati kinahitajika ili kuweka mtindo uliotumika sana ni ule wa ulinganifu wa mizani kumi na sita yaani mizani nane kwa kila mshororo .

- Muhula wa usasa 1967-Mpaka leo

Ni muhula wa mtazamo mpya kimawazo,kisanaa hivyo kuna mgogoro katika uwanja wa ushairi.Katika kipindi hiki washairi walikuwa wanatafuta uhuru wa kisanaa.Mgogogro juu ya kanuni za uandishi wa ushairi uliongezeka kati ya uandishi wa maishairi ya kimapokeo na mashairi ya kisasa.

(Hoja nne@2.5)

Swali la 04

b) Muundo – Jinsi ya upangaji wa visa na matukio katika kazi ya fasihi. Katika kisa hiki, muundo ni wa moja kwa moja (**msago**). Kisa cha mgogoro kati ya Bwana Haji na Yusufu kimepangiliwa kuanzia mwanzi hadi mwisho. (**alama 02**)

c) Mtindo – Namna/mbinu alizotumia mtunzi kuunda kazi yake. Katika kisa hiki, mtunzi ametumia:

(i) Majibizano/daiyalojia mf. kati ya Yusufu na wateja na Yusufu na Haji

(ii) Matumizi ya nafsi ya I (mf. Nitakushtaki ...) **na II** (aliyehodhi bei...) (**alama 02**)

d) Mandhari – Mahali ambapo kazi ya fasihi hufanyika. Katika kisa hiki mandhari ni ya dukani kwa Bwana Haji (mandhari halisi) (**alama 01**)

e) Wahusika – Viumbe ambao mtunzi huwatumia kufikisha ujumbe wake. Katika kisa hiki wahusika ni haji, Yusufu, wateja na mashuhuda wa tukio la ugomvi. (**alama 02**)

f) Matumizi ya lugha – Namna/jinsi lugha ilivyotumika katika kazi ya fasihi. Katika kisa hiki matumizi ya lugha ni kama ifuatavyo:

(i) Tamathali za semi:

- **Tashbiha:** Tamathali inayotumika kufananisha vitu kwa kutumia viunganishi k.v. mfano wa, mithili ya, kana kwamba; ,mf. Unanikazi macho mithili ya kungwi anayemfunda mwali kwa ishara
- **Takriri:** Tamathali ya kurudiarudia maneno, maneno kama Haji, Yusufu
- **Nidaa:** lo!, masalale

(ii) Semi:

- **Methali:** mali bila daftari hughibu bila ya habari
- **Nahau:** kuvimba kichwa
- **Misemo:** Nazi haiwezi kushindana na jiwe (**alama 02**)

Migogoro – Kutokuelewana kati ya pande mbili kutokana na maslahi ya kila upande, mf. Mgogoro kati ya Haji na Yusufu. (alama 01)

5.Utangulizi – maana ya ushairi na madoido na maelezo mengine kuhusu ushairi (alama 03)

Kiini – vipengele hivyo ni

- Uwezo wa kukariri hususani usemaji wa ghibu ndio unaoleta mvuto kwa watazamaji , mf. Ngonjera, kughani, mashairi n.k
- Madoido ya vitendo vya mikono , macho, midomo, kunesa, kupandisha na kushusha sauti ili kukubali jambo , maswali yanayoulizwa na majibu yake.

- Maigizo au ngoma zinapochezwa kinachovutia sio tu sauti bali mingenuo na madoidoya ngoma hiyo ndivyo viletavyo mvuto zaidiya Ghani ya ngoma yenyewe kama ni wa chagga na ngoma yao ya Rosi au Irhingi.
- Vitendo mbalimbali vifanyavyo na fanani katika kukamilisha uwasilishaji wake ndivyo viongezavyo madoido hayo tarajiwa katika kunogesha kipera au fani husika.
- Vigelegele au mbinja, kuendana na mikongo sio ya ngoma husika.

Alama 15 @ 3

Hitimisho – maelezo yoyote kuhusu ushairi (alama 02).

Swali la 06

Mtahiniwa athibitishe mwandishi sio mbinafsi kwa kutoa hoja nne(04)katika riwaya alizozisoma

MFADHILI

i.Anaikumbusha jamii suala zima la bidi katika kazi

ii.Kuhamasisha jamii katika uongozi bora

iii.Anasisitiza umuhimu wa mapenzi bora katika jamii

iv.Anakosoa jamii kwamba chuki haifai miongoni mwetu

VUTA N'KUVUTE

i.Kupiga vita matabaka katika jamii

ii.Anahimiza jamii kuhusu ukombozi

iii.Anaelimisha jamii kuhusu umoja na mshikamano

iv.Anaiasa jamii kuhusu mila potofu

KUFIKIRIKA

i.Kuhamasisha jamii kufanya kazi kwa bidi

ii.Anasisitiza jamii kuhusu suala la elimu

iii.Anaelemisha jamii kuhusu dawa za asili katika matibabu

iv.Anazumgumzia suala la bidi katika kazi

USIKU UTAKAPO KWISHA

i.Kukosoa jamii kuhusu mapenzi ya uongo

ii.Jamii iachane na rushwa

iii.Jamii ifanye kazi kwa bidi

iv.Anazumgumzia ukombozi wa kiuchumi

Alama;Utangulizi 2

Kiiini@2 hoja 8=16

Hitimisho 2

7. Mtahiniwa anatakiwa kukanusha kuwa tamthiliya hazijapitwa na wakati bali huelezea mambo mbali mbali yaliyopo katika jamii

NGUZO MAMA

- Uongozi mbaya
- Ukahaba na umalaya
- Umoja na mshikamano
- Dhulumu
- Ukosefu wa ushirikiano

KIVULI KINAISHI

- Rushwa
- Uzalendo
- Imani za kishirikina
- Uongozi mbaya
- Ugumu wa Maisha

MORANI

- Uzurufu
- Rushwa
- Usaliti
- ukosefu wa haki
- uzalendo

Utangulizi alama 02

Kiini hoja 8@2=16

Hitimisho 02

8. Mtahiniwa anatakiwa atoe maana ya mtindo na afafanue mitindo mbali mbali katika tamthiliya alizosoma

MORANI

- Barua
- Masimulizi
- Wimbo ambao uliandalia na jalia na wenzake kwa lengo la kuonesha watenda maovu
- Taarifa ya habari ambayo imejengwa kuonesha maovu
- Tangazo lililotolewa na mgambo kuwataka watu wote waungane na kufanya maaandamano
- Matumizi ya nafsi
- Lugha za Biblia,ELOI ELOI LAMA SABAKITANI
- Matumizi ya nyimbo
- Matumizi ya nafsi
- Majigambo
- Matumizi ya dayalojia
- Matumizi ya masimulizi

KIVULI KINAISHI

- Matumizi ya hadithi
- Matumizi ya dayalojia
- Ushairi
- Matumizi ya nafsi
- Mtindo wa kuyapa maonesho majina

KWENYE UKINGO WA THIM

- Mtindo wa dayalojia
- Nafsi zote tatu
- Ushairi

Utangulizi 02

Hoja 8@2=16

Hitimisho 02